**TAARIFA YA HISTORIA YA MKOA WA MWANZA KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru kimkoa imeandaliwa kwa kuzingatia sehemu za Historia ya mkoa wa Mwanza, Hali ya uongozi na utawala, mafaniko ya maendeleo ya kisekta na matarajio ya mkoa kwa kipindi cha miaka 50 ijayo na namna ya kukabili changamoto za maendeleo.

## 2.0 HISTORIA YA MKOA WA MWANZA

Historia ya mkoa wa Mwanza ilianza wakati ukiwa chini ya tawala za kitemi za wasukuma, wazinza, walongo, wakara na wakerewe kabla ya ukoloni. Wajerumani walipotawala Tanganyika eneo la Mwanza likawa mojawapo ya wilaya katika himaya ya utawala wa Kijerumani. Utawala wa kikoloni wa Mwingereza ulipokabidhiwa uangalizi wa Koloni la Afrika Mashariki baada ya vita kuu ya Dunia, ulianzisha utawala wa majimbo yaani Provinces. Tanganyika ilikuwa na majimbo ya kiutawala manane (8) na mojawapo likiwa ni Lake Province. Lake Province liliundwa kwa kujumuisha maeneo ya wilaya za Mwanza, Biharamulo, Bukoba, Maswa, shinyanga, Musoma na Kwimba. Baadaye Lake Province liligawanywa na kuunda majimbo mawili la Lake Province (Sukuma Land) na Western Province). Utawala wa Mwingereza ulimalizika na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961. Baada ya uhuru Mwanza iliendelea kuwa sehemu ya Jimbo la Lake Province chini ya mtawala wake kwanza wa jimbo (Provincial Commissioner) aliyeitwa Provincial Commissioner Bw. Walden, ambaye alikabidhi madaraka kwa Richard Wambura.

Mkoa wa Mwanza ulianzishwa rasmi mwaka 1963 ukiwa na wilaya nne za Ukerewe, Geita, Mwanza na Kwimba. Mwaka 1972 baada ya sera ya madaraka mikoani wilaya zaidi zilianzishwa kwa kuanza na Magu mwaka 1974. Wilaya ya Sengerema ilianzishwa mwaka 1975 ambapo awali ilikuwa ni tarafa mojawapo ya wilaya ya Geita. Misungwi ilianzishwa mwaka 1995 ambapo awali ilikuwa ni eneo la tarafa za wilaya ya Kwimba, Ilemela na Nyamagana zilianzishwa mwaka 2002 ambazo zilikuwa zinaunda wilaya ya Mwanza. Mwaka 2010 mikoa mipya ya Geita na Simiyu ilitangazwa kuanzishwa. Wilaya mpya pia za Busega na Nyanghwale nazo zilitangazwa kuanzishwa 2010 na utekelezaji wake utaanza rasmi wakati wowote katika mwaka wa fedha 2011/12.

## 3.0 HALI YA UONGOZI NA UTAWALA

### 3.1 MAENEO YA UTAWALA

Mkoa wa Mwanza uko kaskazini Magharibi ya Tanzania, kusini mwa Ziwa Victoria, umepakana na mkoa wa Kagera kwa upande wa magharibi, Shinyanga kwa upande wa kusini na kusini mashariki, kwa upande wa kaskazini na kaskazini mashariki, mkoa umepakana na mkoa wa Mara. Mkoa uko kati ya latitudo 1º 30' na 3º 0' kusini mwa Ikweta kaskazini mwa Tanzania, na Longitudo 31º 45 na 34º 10' mashariki ya mstari wa Grinwichi. Mkoa una wilaya 8, halmashauri 7, ikiwemo jiji la Mwanza linalohudumia wilaya za Ilemela na Nyamagana. Mkoa una majimbo ya uchaguzi 13, tarafa 33, kata 214 na vijiji 740. kwa ongezeko la maoteo ya sensa ya mwaka 2002 mkoa unakadiriwa kuwa na jumla ya watu 3,669,380.

| | Wilaya | Halmashauri | Ukubwa wa maeneo | | | Maeneo ya utawala | | | | | Idadi ya watu 2011 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Nchi kavu | Maji | Jumla | Majimbo ya uchaguzi | Tarafa | Kata | Vijiji | Mitaa/ vitongoji | |
| 1 | Magu | Magu | 3,070 | 1,725 | 4,795 | 2 | 6 | 27 | 124 | 763 | 517,373 |
| 2 | Ukerewe | Ukerewe | 640 | 5,760 | 6,400 | 1 | 4 | 24 | 74 | 509 | 328,207 |
| 3 | Geita | Geita | 6,775 | 1,050 | 7,825 | 3 | 7 | 33 | 213 | 859 | 879,836 |
| 4 | Sengerema | Sengerema | 3,335 | 5,482 | 8,817 | 2 | 5 | 25 | 126 | 766 | 622,366 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Kwimba | Kwimba | 3,903 | - | 3,903 | 2 | 5 | 25 | 117 | 802 | 387,562 |
| 6 | Misungwi | Misungwi | 1,947 | 175 | 2,122 | 1 | 4 | 27 | 86 | 625 | 316,672 |
| 7 | Nyamagan a | Jiji mwanza | 173 | 83 | 256 | 1 | 1 | 12 | - | 265 | 275,122 |
| 8 | Ilemela | Jiji Mwanza | 252 | 817 | 1,069 | 1 | 1 | 9 | - | 140 | 342,242 |
| | | **JUMLA:** | **20,095** | **15,092** | **35,187** | **13** | **33** | **214** | **740** | **4729** | **3,669,380** |

## 3.2 ORODHA YA VIONGOZI WA MKOA

WAKUU WA MKOA WA MWANZA 1961 – 2011:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Richard | Wambura | 1961 - 1963 |
| 2. Mhe. John | Samwel Malecela | 1963 – 1965 |
| 3. Mhe. Joseph | Nyerere | 1965 – 1967 |
| 4. Mhe. Joseph | Namata | 1967 – 1969 |
| 5. Mhe. Omari | Muhaji | 1970 – 1972 |
| 6. Mhe. Lawi | Sijaona | 1972 – 1975 |
| 7. Mhe. Peter | Kisumo | 1975 – 1977 |
| 8. Mhe. Muhidini | Kimario | 1977 - 1979 |
| 9. Mhe. Abdulnuru | Suleiman | 1979 – 1981 |
| 10. Mhe. Daniel | Machemba | 1981 – 1987 |
| 11. Mhe. Timoth | Shindika | 1987 – 1992 |
| 12. Mhe. Philip | Mangula | 1992 - 1993 |
| 13. Mhe. Ernest | Nyanda | 1993 – 1994 |
| 14. Mhe. William | Shija | 1994 – 1995 |
| 15. Mhe. Maj. Gen. James | Luhanga | 1996 – 1999 |
| 16. Mhe. Stephen J. | Mashishanga | 1999 – 2003 |
| 17. Mhe. Daniel Ole | Njoolay | 2003 – 2006 |
| 18. Mhe. Dr. James A. | Msekela | 2006 – 2009 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19. Mhe. Abbas | H. | Kandoro | 2009 – 2011 |
| 20. Mhe. Eng. Evarist | W. | Ndikilo | 2011- |

WAKURUGENZI WA MAENDELEO MKOA (RDD) NA MAKATIBU TAWALA WA MKOA WA MWANZA 1961-2011

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Bw. C.T.L. | | Scoti | 1960 – 1961 |
| 2. Bw. A.G. | | Stephen | 1961 – 1965 |
| 3. Bw. J.P. | | Singano | 1965 – 1968 |
| 4. Bw. S.J. | | Galinoma | 1968 - 1972 |
| 5. Bw. C.Y. | | Mpupua | 1972 – 1975 |
| 6. Bw Raphael. | | Lukindo | 1975 – 1976 |
| 7. Bw. D. F .P .D. | | Ringo | 1976 – 1977 |
| 8. Bw. W.K. | | Kasera | 1977 – 1981 |
| 9. Bw. William | H. | Shelukindo | 1981 – 1984 |
| 10. Bw. John | K. | Kyambwa | 1984 – 1985 |
| 11. Bw. Edward | O. | Oluoch | 1985 – 1987 |
| 12. Bw. Michael | D. | Mapunda | 1987 – 1990 |
| 13. Bw. John | K. | Kyambwa | 1990 – 1995 |
| 14. Bw. Rajab | R. | Kiravu | 1995 – 1997 |
| 15. Bw. Clemence | M. | Rutaihwa | 1997 – 2006 |
| 16. Alhaj Yahaya | F. | Mbilla | 2006 – 2008 |
| 17. Bi. Dorothy | S. | Mwanyika | 2009 – |

## 3.3 MAJUKUMU YA SERIKALI KATIKA MKOA

Majukumu ya mkoa kwa wananchi,taasisi na mamlaka za serikali katika mkoa ni yale yanayotekelezwa kupitia sheria, miongozo na taratibu za uendeshaji kazi serikalini na uanzishwaji wa mamlaka ama taasisi hizo za serikali. Kwa mujibu wa Ibara ya 61 (1) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Mkuu wa Mkoa atakuwa ndiye Mkuu wa utekelezaji wa kazi zote za Serikali katika Mkoa aliochaguliwa kuuongoza kwa mujibu wa Sheria.

MKUU WA MKOA

Uhusiano wa Mkuu wa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, upo katika majukumu ya Mkuu wa Mkoa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya na miji) Sura 287 na 288 pamoja na kifungu cha 5 (1)- (3) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97 (awali sheria na. 19 ya mwaka 1997) kama yafuatayo:-

- Kuhakikisha panapatikana utulivu na amani katika Mkoa,
- Kuwezesha Kuidhinisha Sheria ndogo za Mamlaka za Miji na Wilaya,
- Kuchunguza uhalali wa matendo na maamuzi ya Serikali za Mitaa katika mkoa wake iwapo yametiliwa mashaka na kuchukua hatua ifaayo kwa kumjulisha Waziri,
- Kutoa idhini kwa mtu yeyote kimaandishi kukagua vitabu vyote vya hesabu vya Halmashauri na kumbukumbu za Halmashauri,
- Kuelekeza Serikali za Mitaa namna ya kutangaza mizania ya hesabu zake na taarifa yoyote iliyotolewa na Mkaguzi wa nje juu ya hesabu za mwaka za Halmashauri,
- Kuelekeza nguvu iwekwe wapi katika utekelezaji wa Sera za Serikali,
- Kuwezesha na kusaidia mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya kuziwezesha kutekeleza kazi na majukumu yao,
- Kwa kupitia Kamati ya Ushauri ya Mkoa, kutoa ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu mipango yao ya maendeleo;
- Kupokea mihtasari ya Halmashauri kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 155 (3) cha Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 287, Mkuu wa Mkoa amepewa jukumu la kupitia Sheria ndogo ya Halmashauri za Wilaya na kuzitolea maoni kabla hazijawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kuidhinishwa.

KATIBU TAWALA WA MKOA

Nafasi ya Katibu Tawala wa Mkoa imeainishwa kwenye kifungu cha 12 (1) – (3) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Sura ya 97. Katibu Tawala Mkoa (RAS) ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za serikali katika mkoa. Uhusiano wa Katibu Tawala wa Mkoa na Mamlaka

za Serikali za Mitaa upo katika wajibu wa Katibu Tawala Mkoa katika kusimamia shughuli za mamlaka za Serikali za Mitaa.



*KatibuTawala Mkoa wa Mwanza Bi. Dorothy S. Mwanyika akiwa katika safari za kikazi kisiwa cha ukara wilayani Ukerewe*

Uhusiano huu unaonekana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya seksheni zilizopo kwenye Sekretarieti za Mikoa ambazo Katibu Tawala wa Mkoa ndiye Mkuu wa Sekretarieti hiyo. Hivyo, wajibu wake ni kuhakikisha Sekretarieti ya Mkoa inatimiza wajibu wa kuzishauri, kuzielekeza na kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yafuatayo:-

- Kuhakikisha Sekretarieti ya Mkoa inazishauri Halmashauri katika Nyanja za Sheria, Uchumi, Takwimu, Maendeleo ya Jamii, Afya, Elimu, utekelezaji wa Sera

na sheria zinazopelekwa Halmashauri zinazohusu Uchumi, Takwimu, Maendeleo ya Jamii, Afya na Elimu kwa kupitia watalaam wa seksheni.

- kuhakikisha Sekretarieti ya Mkoa inazishauri Halmashauri katika Nyanja za usimamizi wa fedha na kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye usimamizi wa utawala na rasilimali watu, Sheria, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala, kuboresha Utawala Bora, kufanya ukaguzi ili kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- Kwa kupitia vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa hutumia nafasi hiyo kutoa ushauri wa kitaalam katika upangaji wa mipango na utekelezaji wake.

Sekretarieti ya Mkoa ambayo hujumuisha sehemu zenye wataalam waliobobea katika fani mbalimbali (**think tank)**, ni chombo na kitovu cha uwezo, taaluma na ujuzi wa kutoa tafsiri sahihi ya Sheria, Kanuni, Miongozo, Sera, Mikakati, Mipango, Miradi na Maamuzi mbalimbali ya Serikali kuhusu maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

Majukumu ya Sekretarieti ya mkoa kuhusiana na Serikali za Mitaa yameanishwa chini ya kifungu cha 9 (1) – (f) cha sheria ya Tawala za mikoa Sura 97, ambayo ni haya yafuatayo:-

- Kupitia Bajeti ya Halmashauri na kutoa ushauri kuhusu Sera za Taifa, mipango ya kitaifa na Kanuni za fedha kwa kila Mkurugenzi wa Halmashauri ili masuala hayo yazingatiwe katika bajeti za Halmashauri.
- Kuunganisha mipango na bajeti za Halmashauri zilizo katika mkoa na kuziwasilisha kwenye ngazi ya kitaifa ili zijadiliwe na kutolewa fedha,
- Kuchambua na kuunganisha bajeti za Halmashauri za robo mwaka za utekelezaji wa mipango na matumizi ya fedha na kuziwasilisha kwenye Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa pamoja na maoni ya Sekretarieti ya Mkoa.
- Kufuatilia na kutathmini matumizi ya ruzuku ya Serikali za Mitaa zilizo katika mkoa.
- Kufuatilia na kutoa ushauri kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu masuala ya maendeleo katika mamlaka hizo.

MKUU WA WILAYA

Uhusiano wa Mkuu wa wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni katika majukumu ya Mkuu wa Wilaya kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288 (Mamlaka za wilaya na Miji) na kifungu Na. 14(3) (a) – (c) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Sura 97 kama yafuatayo:-

- Kuhakikisha kuwa kuna utulivu na amani katika Wilaya
- Kuziwezesha na kuzisaidia Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa kuweka mazingira mazuri ya kutekeleza kazi zake.
- Kuhakikisha watu wote na mamlaka zote zinatekeleza maamuzi, miongozo na Kanuni za Serikali mintarafu ukuzaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa,
- Kuchunguza uhalali wa matendo na maamuzi ya Serikali za Mitaa zilizo katika wilaya yake iwapo yametiliwa mashaka na kuchukua hatua ifaayo kwa kumjulisha Waziri;
- Kupokea mihtasari ya Halmashauri kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri,
- Kumwagiza kimaandishi mtumishi yeyote wa Halmashauri aliye katika vazi rasmi kumkamata mtu anayevunja sheria ndogo ya Halmashauri mbele yake.

Mkuu wa Wilaya pamoja na kuwa na madaraka ya jumla yanayotiririka kutoka kwa Rais kupitia kwa Mkuu wa Mkoa, ni Msaidizi Mkuu wa Mkuu wa Mkoa na ana wajibu wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Serikali katika eneo la wilaya aliyokabidhiwa aiongoze. Katika kutekeleza majukumu yake Mkuu wa wilaya anatakiwa kuzingatia Katiba, Sera za kitaifa, Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Mkuu wa Wilaya ni mwakilishi wa Serikali Kuu katika wilaya aliyoteuliwa kuongoza, anawajibika kujenga mazingira ambayo yataziwezesha Serikali za mitaa kufanya kazi kwa ufanisi na tija bila kuingiliwa na mamlaka au chombo kingine chochote katika eneo la wilaya husika. Mkuu wa Wilaya anapaswa kuhakikisha kuwa ulinzi, usalama, amani na utulivu vinakuwepo katika wilaya kwa shabaha ya kuwajengea wananchi mazingira

ya kutekeleza kazi za uzalishaji mali na huduma kwa manufaa ya maendeleo yao na ya wilaya.

Ili kuwezesha Mkuu wa wilaya kutekeleza kikamilifu majukumu yake, Sheria ya Tawala za Mikoa imempa madaraka ya kuwa mlinzi wa amani (**Justice of Peace**) na anaweza kukamata au kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote ambaye anafanya au kunuia kufanya vitendo vya kuhatarisha amani katika eneo la Wilaya yake kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Sheria hususan katika suala la kuweka kizuizini anayeridhika kwamba vitendo vyake vinaweza kupelekea kuvunjika kwa amani.

Mkuu wa Wilaya ana majukumu mengine yafuatayo:-

- Kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Mipango yote ya Serikali katika eneo lake kama vile MMEM, MES, DADPS, ASPD,MAM, n.k.
- Kuhakikisha kuwa kila mwananchi, Taasisi au chombo chochote chenye mamlaka au wajibu wa kufanya shughuli katika eneo lake vinazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Maamuzi na Miongozo yote ya Serikali kikamilifu.
- Mkuu wa Wilaya amepewa mamlaka ya Msajili wa Ndoa katika wilaya ambayo ameteuliwa kufanya kazi. Msajili wa ndoa anayo madaraka ya kufungisha ndoa za watu ambao wana sifa zinazotakiwa kisheria kuingia katika maisha ya ndoa kama kifungu cha 13 (1) cha sheria ya ndoa sura 29 kinavyoelekeza.
- Mkuu wa wilaya ana wajibu wa kufanya jambo au shughuli yoyote ambayo inaweka mazingira ya ufanisi na tija katika utendaji kazi wa Serikali au mamlaka nyingine katika eneo lake. Kwa tafsiri ya mamlaka na wajibu aliopewa Mkuu wa Wilaya anaweza kusimamia na kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka kama vile kusimamia vita dhidi ya UKIMWI, Utawala Bora, Utawala wa Sheria, hifadhi ya mazingira, maendeleo ya jinsia, vita dhiti ya rushwa na kuzuia matukio ya maafa mbalimbali ambayo yanaweza kutokea katika Wilaya yake.
- Mkuu wa Wilaya anatakiwa awe chachu ya mabadiliko (change agent) katika eneo lake. Ili aweze kuwa chachu ya mabadiliko anapaswa aelewe nadharia,

misingi na maudhui ya mabadiliko kama yanavyowekwa katika Sera na mikakati inayoandaliwa na kupitishwa na Serikali.

- Kifungu cha 30 (4) kinampa uwezo Mkuu wa Wilaya kupokea rufaa ya Mwenyekiti wa Kitongoji aliyeondolewa madarakani.
- Kifungu cha 59 (2) kinampa uwezo Mkuu wa wilaya kupokea rufaa ya Mwenyekiti wa Kijiji aliyeondolewa madarakani na theluthi mbili ya wajumbe wa mkutano mkuu wa Kijiji.
- Kifungu cha 184 kinamruhusu Mkuu wa wilaya kutoa ruhusa kwa mtumishi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa au afisa yeyote wa Halmashauri aliyevaa sare kumkamata mtu yeyote anayefanya kosa mbele yake au kuvunja sheria ndogo ya Halmashauri ya wilaya au ya Mji mdogo na anaweza, ikiwa ataelekezwa na Mkuu wa wilaya hiyo kumweka rumande mtu huyo kwa muda unaofaa kwa ajili ya kumfikisha Mahakamani kwa mujibu wa sheria.




***Jengo la Halmashauri ya Jiji la Mwanza mkoani Mwanza***

KATIBU TAWALA WA WILAYA

Katibu Tawala wa wilaya ametambuliwa na Sheria ya Tawala za Mikoa katika sura ya 97 chini ya kifungu cha 16 (1). Kifungu hicho kinasema, atateuliwa au kupelekwa kwenye kila wilaya ya Tanzania Bara kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi, Afisa wa Serikali mwenye wadhifa wa Katibu Tawala wa wilaya.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa sura ya 97, kifungu cha 16 (2) na (3), ikisomwa pamoja na taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa Umma za mwaka 2003, kifungu cha 9 (3), kwamba Katibu Tawala wa Wilaya ndiye msimamizi wa Serikali za Mitaa wilayani katika kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:-

- Kuzishauri Serikali za Mitaa kusimamia na kutekeleza sheria mbalimbali za Utumishi wa Umma
- Kuzishauri Serikali za Mitaa kusimamia Kanuni mbalimbali zinazotolewa na Serikali Kuu.
- Kuzishauri Serikali za Mitaa kusimamia maagizo mbalimbali yanayotolewa na Serikali Kuu,
- Kuzishauri Serikali za Mitaa kusimamia maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Serikali kuu.

KAMATI YA USHAURI YA WILAYA

Kamati ya mashauriano ya Wilaya ambayo inaundwa chini ya kifungu cha 15A cha marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 13 ya mwaka 2006 ina majukumu yafuatayo:-

- Kupokea taarifa, kujadili na kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri,
- Kushauri Mkoa kuhusu miradi ya maendeleo ya kitaifa inayotekelezwa wilayani;
- Kutoa ushauri juu ya shughuli za mashirika ya umma, vyama vya ushirika na Taasisi nyingine zisizo za Serikali katika wilaya,

- Kuzishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza maamuzi ya Halmashauri na Serikali Kuu.
- Kuhakikisha kuwa maadili ya vyama vya siasa yanafuatwa na kuzingatiwa kwa madhumuni ya kuwa na amani na utulivu katika wilaya husika,
- Kuratibu na kushughulikia maafa ikiwa ni pamoja na matetemeko ya ardhi, mafuriko, ukame, mioto, njaa na milipuko ya magonjwa.
- Kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi ya Halmashauri.



***Jengo la Halmashauri ya wilaya ya ukerewe Mkoani Mwanza***

AFISA TARAFA

Mwaka 1962 utawala wa watemi ulifutwa na maeneo ya utemi kuitwa rasmi Tarafa. Nafasi ya Afisa Tarafa imeainishwa katika kifungu cha 31 (1) cha marekebisho ya sheria za Serikali za Mitaa Na. 13 za mwaka 2006 (Local Government Miscellineous Amendments Act of 2006).

Majukumu ya Maafisa Tarafa:

- Kumwakilisha na kumsaidia Mkuu wa wilaya katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika eneo lake;

- Kuandaa na kuratibu taarifa za hali ya ulinzi na usalama kwa kata zilizopo katika eneo lake na kutoa taarifa kwa Mkuu wa wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri.
- Kufuatilia na kuhimiza utekelezaji wa Sera za Serikali katika eneo lake na kuhakikisha zinatekelezwa ipasavyo
- Kufuatilia na kuhimiza utekelezaji wa shughuli za maendeleo.
- Kuwa kiungo kati ya wananchi na Serikali katika eneo lake.
- Kuratibu shughuli zote za kupambana na maafa na dharura mbalimbali katika eneo lake.
- Kuandaa taarifa zinazohusu masuala ya Serikali Kuu katika eneo lake na kuwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya.
- Kuwa kiungo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika eneo lake;
- Kuratibu na kuandaa taarifa za pamoja kwa Kata zote zilizo katika eneo lake na kuziwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.
- Kufanya kazi nyingine kama atakavyoagizwa na Mkuu wa wilaya/Katibu Tawala wilaya
- Kuhakikisha utekelezaji wa masuala na maamuzi ya kisiasa toka Serikali Kuu katika Tarafa yake.

Aidha, uhusiano wa Afisa Tarafa na Mamlaka za Serikali za Mitaa upo kwa mujibu wa kifungu Na. 31 (b) cha marekebisho Na. 13 ya sheria za Serikali za Mitaa za mwaka 2006 ambapo anawajibika kwa Mkurugenzi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenye jambo lolote linalohusu maendeleo ya Tarafa husika.

Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 1 wa mwaka 2007 unaohusu Muundo wa Utumishi wa Maafisa Tarafa, uliotolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma wenye Kumb. Na. AC.260/431/01/7 wa tarehe 01/07/2007 uliainisha majukumu ya Afisa Tarafa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:-

- Kuwasaidia Wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia maendeleo ya eneo lake.

- Kusimamia utendaji wa shughuli za maafisa watendaji wa Kata na Mitaa;
- Kushiriki na kutoa ushauri kuhusu upangaji wa mipango ya maendeleo katika eneo lake.
- Kuratibu vikao vya Kamati za kudumu za Baraza la Madiwani vya Halmashauri na kutoa ushauri.
- Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake kama zitakavyopokelewa kutoka kwa Watendaji wa Kata.
- Kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo za Halmashauri za Wilaya, MijiManispaa na Majiji.

### 3.4 MUUNDO WA SEKRETARIETI YA MKOA

Sekretarieti ya Mkoa asili yake ni sera ya Taifa ya kupeleka madaraka karibu na wananchi ya mwaka 1972. Kimsingi sera hii ilisogeza madaraka ya kiwizara mikoani na kutekelezwa chini ya Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa (RDD). Katika muundo huu wataalam waliajiriwa na Wizara mama na RDD aliajiri watumishi mwisho ngazi ya mshahara GS 2.

Mnamo mwaka 1996 ofisi ya RDD ilisitishwa na nafasi yake kuchukuliwa na ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Sheria Na. 19 ya mwaka 1997 ya Tawala za Mikoa ilihalalisha uanzishwaji wa ofisi ya Katibu Tawala Mkoa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu. Mnamo Novemba 1998 Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliundwa na ofisi ya Katibu Tawala kuwa chini ya Wizara hiyo.

Hata hivyo mnamo Januari 2000 Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilihamishiwa Ofisi ya Rais na kujulikana kama OR-TAMISEMI (PORALG). Mwaka 2002 muundo wa Tawala za mikoa wenye idara ulifanyiwa tathmini na kuwa na seksheni ambazo ziliwajibika kwa Katibu Tawala Mkoa. Katika awamu ya nne ya uongozi Januari 2006 TAMISEMI ilirudishwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO-RALG).

Lengo la mabadiliko haya yote ilikuwa ni kupeleka madaraka karibu zaidi na wananchi. Hata hivyo ofisi ya RDD na Serikali za mitaa zilizorejeshwa mwaka 1984 zilikuwa na mwingiliano (Mgongano) kwenye shughuli zake za kila siku kwa kuwa zote zilikuwa zinatekeleza sheria Na. 7 na Na. 8 ya mwaka 1982 na kwa kufanya hivyo kulikuwa na athari za kimaendeleo.

Mnamo mwaka 2007 kwa mara nyingine Muundo sekretarieti za mikoa wenye ***clusters*** ulifanyiwa tathmini na kuundwa "Sehemu" (Seksheni) na "VITENGO" (Units) na ndio unaotumika wakati huu wenye mfumo wa kiidara katika mkoa. Muundo huu umefanyiwa marekebisho ya maboresho mwezi Juni 2011 ili kuwezesha Sekretarieti ya Mkoa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Muundo huu utawezesha RS na vitengo vyake kuwa na watumishi 146 kama ifuatavyo:-

1. Sehemu/seksheni ya Mipango na Uratibu -8
2. Sehemu ya Huduma za jamii na afya-8
3. Sehemu ya Uchumi na uzalishaji-19
4. Sehemu ya Miundombinu-9
5. Sehemu ya Menejimenti ya Huduma za Serikali za Mitaa-10
6. Sehemu ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu-54
7. Kitengo cha Fedha na uhasibu-12
8. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani-3
9. Kitengo cha Menejimenti ya Manunuzi-3
10. Kitengo cha Mkuu wa wilaya(DAS)-18
11. Ofisi ya Tarafa-5
12. Seksheni ya huduma za maji-5
13. Kitengo cha Sheria-2
14. Seksheni ya elimu-7
15. Kitengo cha habari na mawasiliano-6

# THE ORGANIZATIONAL STRUCTURE FOR REGIONAL SECRETARIATS

***(Approved by the President on 3rd June, 2011)***



### 3.5 HALI YA ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama mkoani Mwanza kabla ya uhuru ilikuwa ya uhakika sana kwa sababu lilikuwa ni jukumu la jamii nzima. Chombo cha kutoa haki wakati huo kilikuwa ni vikao vya wanangwa au watemi. Wanangwa walitokana na watu walioaminiwa kuongoza na wana uwezo wa kuleta mvua, hivyo haikuwa rahisi kuwepo uvunjifu wa amani. Hali hii imeendelezwa hata baada ya uhuru mwaka 1961 ambapo jamii ilianzisha ulinzi wa jadi wa sungusungu katika vijiji na vitongoji vyote. Mwaka 2011 kutokana na maendeleo makubwa yaliyopatikana katika maeneo ya vijijini, mijini na kwenye majiji kulikoendana na ongezeko la watu wanaoendesha shughuli za uzalishaji mali pamoja na uwepo wa vyombo vya usalama vya serikali, jeshi letu la polisi limekuja na dhana ya ulinzi shirikishi na polisi jamii. Hali hiyo imewezesha mkoa kuwa na amani na utulivu. Mwaka 1961 kulianzishwa kisheria mamlaka mbalimbali zinazotawala na kusimamia usalama na ulinzi wa mkoa. Mkoa una vituo vikuu vya polisi vya wilaya vipatavyo 9, magereza yapatayo 7, mahakama za wilaya zipatazo 8. Vituo vidogo vya polisi na mahakama za mwanzo vimeanzishwa hadi katika ngazi za Tarafa na kata waliko wananchi wengi. Jeshi letu la mgambo kila mwaka limeongeza mafunzo kwa wanamgambo katika kila wilaya. Madhumini ya msingi ya vyombo hivi ni kupambana na kuzuia uhalifu bila kuathiri hali ya usalama wa raia na mali zao.



*Jeshi la Sungusungu katika shughuli za ulinzi Wilayani Kwimba Mkoani Mwanza.*

Uwepo wa utulivu na amani umewezesha Mkoa wa Mwanza kupata mafanikio katika sekta za uzalishaji na uchumi, sekta ya huduma za jamii za afya, elimu, maji, maendeleo ya vijana, miundombinu, hasa mabarabara, usafiri majini na anga, maendeleo ya ardhi na urasimishaji wa makazi na mashamba. Nchi yetu imepiga hatua katika nyanja za utawala bora na haki za binadamu na usimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa ambazo zinaongozwa na wananchi wenyewe kupitia wawakilishi viongozi waliowachagua katika ngazi mbalimbali za utawala.

### 3.6 HALI YA KISIASA

Mkoa wa Mwanza una majimbo ya Uchaguzi wa viti vya Ubunge 13 na Kata 214. Jedwali lifuatalo linaonyesha majina ya Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza pamoja na Majimbo yao na vyama wanavyotoka. Mwaka 1961 mfumo wa vyama vingi ulikuwepo ambapo ulisitishwa na kuweka mfumo wa chama kimoja cha TANU iliyozaa CCM mwaka 1977. Mwaka 1992 mfumo huo ulirejeshwa nchini. Katika mkoa wa mwanza hivi leo mwaka 2011 kuna vyama vya siasa vya CCM, CHADEMA, TLP, CUF, NCCR-MAGEUZI, na UDP.

Mkoa una jumla ya Waheshimiwa Madiwani 289, wakiwemo Madiwani 214 wa kuchaguliwa katika Kata zao na waheshimiwa Madiwani 75 wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Jedwali la Idadi ya Madiwani na vyama wanavyotoka kwa kipindi cha 2010-2015

| **Kuchaguliwa** | | **Viti maalum** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Chama | Madiwani | Chama | Madiwani | |
| CCM | 162 | CCM | 58 | 220 |
| CUF | 10 | CUF | 2 | 12 |
| CHADEMA | 35 | CHADEMA | 13 | 48 |
| UDP | 7 | UDP | 2 | 9 |
| **JUMLA** | **214** | | **75** | **289** |

Waheshimiwa Wabunge na Majimbo na vyama watokavyo kipindi 2010-2015

| Na. | Jina | Chama | Jimbo | Wilaya |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dr. Festus Limbu | CCM | Magu | Magu |
| 2. | Dr.Kamani  Mlengeya | CCM | Busega | Magu |
| 3. | Richard Ndassa | CCM | Sumve | Kwimba |
| 4. | Mansoor Sharif Hiran | CCM | Kwimba | Kwimba |
| 5. | Charles Kitwanga | CCM | Misungwi | Misungwi |
| 6. | William Ngeleja | CCM | Sengerema | Sengerema |
| 7. | Tizeba Charles | CCM | Buchosa | Sengerema |
| 8. | Hussein Nasor Awar | CCM | Nyang'hwale | Geita |
| 9. | Max Donald | CCM | Geita | Geita |
| 10. | Lolesia Bukwimba | CCM | Busanda | Geita |
| 11. | Wenje D. Ezekia | CHADEMA | Nyamagana | Nyamagana |
| 12. | Haines S, Kiwia | CHADEMA | Ilemela | Ilemela |
| 13. | Salvatory  Machemli | CHADEMA | Ukerewe | Ukerewe |
| 14. | Josephine Chagula | CCM | Viti Maalum | |
| 15. | Maria Hewa | CCM | Viti Maalum | |
| 16. | Vicky Kamata | CCM | Viti Maalum | |
| 17. | Leticia Nyerere | CHADEMA | Viti Maalum | |

## 4.0 MAFANIKIO YA MAENDELEO YA KISEKTA KUANZIA 1961-2011

### 4.1 HALI YA UCHUMI YA MKOA WA MWANZA

Shughuli kuu za kichumi na uzalishaji katika mkoa wa Mwanza tangu wakati wa uhuru ni biashara, kilimo cha pamba, kilimo cha mazao, madini, uvuvi, ufugaji na ajira mbalimbali zitokanazo na shughuli za viwanda, mabenki, NGOs, serikalini,na sekta binafsi.

Ukuaji wa uchumi mkoa wa Mwanza

| Mwaka | Makadirio ya idadi ya watu | Uchumi wa mkoa (RGDP) | Wastani wa pato la mtu kimkoa |
|---|---|---|---|
| 2001 | 2,631,866 | 813,465,000 | 309,083 |
| 2002 | 2,942,148 | 948,526,000 | 322,392 |
| 2003 | 3,008,570 | 958,338,000 | 318,536 |
| 2004 | 3,106,401 | 1,105,256,000 | 355,799 |
| 2005 | 3,196,714 | 1,231,646,000 | 385.255 |
| 2006 | 3,168,904 | 1,405,259,000 | 443,454 |
| 2007 | 3,265,730 | 1,642,748,000 | 503,026 |
| 2008 | 3,364,378 | 1,953,307,000 | 580,688 |
| 2009 | 3,464,567 | 2,594,150,000 | 748,766 |
| 2010 | 3,566,263 | 2,958,739,000 | 829,647 |
| 2011 | 3,566,263 | zinakusanywa | zinakusanywa |

## 4.2 KILIMO

Kabla na wakati wa uhuru kilimo kilikuwa kwa kila kaya kujilimia mazao ya chakula kwa ajili ya kutosheleza na kuchangia katika maghala ya watemi. Mazao ya chakula yaliyolimwa yalikuwa ni mtama, viazi, mhogo, ulezi na migomba katika baadhi ya maeneo. Zao la biashara la pamba ilikuwa ni lazima kupandwa na kila mkulima, asiyepanda alichukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa pamoja na kifungo. Pia, kulikuwa na kilimo cha zao la katani(mkonge) kwa baadhi ya maeneo. Mkoa wa Mwanza kwa kufuata utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala tangu TANU na sasa CCM, serikali imeweza kutekeleza kwa kasi nzuri mageuzi ya kilimo ikiwa pamoja na kukabiliana na changamoto za sekta hii.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasisitiza umuhimu wa kilimo cha kisasa na chenye tija kwa uchumi wa kisasa. Mkoa umeweka mwongozo wa mapinduzi ya kilimo unaolandana na

mwongozo wa Taifa wa kilimo kwanza. Mwongozo huu wa mkoa ni *Ondoa Njaa Mkoani Mwanza*. Lengo ni kutumia fursa za maji ya Ziwa Victoria na vyanzo vingine kwa kilimo cha umwagiliaji na pia idadi kubwa ya wanyamakazi ili kujitosheleza kwa chakula. Jitihada hizo zimeuletea mkoa mafanikio makubwa katika kilimo cha pamba, mpunga, mhogo, choroko, dengu, mbogamboga na viazi vitamu.

ENEO LA KILIMO

| Wilaya | Ardhi iliyopo (Ha) | Eneo linalofaa kilimo(Ha) | Eneo linalolimwa (Ha) | % |
|---|---|---|---|---|
| Geita | 6,775 | 458,200 | 198,005 | 43.2 |
| Sengerema | 3,335 | 274,900 | 117,932 | 42.9 |
| Kwimba | 3,903 | 411,600 | 158,894 | 38.6 |
| Misungwi | 1,947 | 135,800 | 87,192 | 64.4 |
| Magu | 3,070 | 286,800 | 115,189 | 40.2 |
| Ilemela na Nyamagana | 425 | 2,730 | 14,051 | 51.1 |
| Ukerewe | 640 | 63,200 | 50,368 | 79.4 |
| **JUMLA:** | **20,095** | **1,657,800** | **741,631** | **44.7** |

Katika kipindi cha miaka 50 ya uhuru bajeti ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo imeongezeka hadi kufikia Tshs. 6,168,900,816 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 1,051. Kufuatia ongezeko hilo manufaa ya moja kwa moja ya wakulima binafsi (mkulima mmoja mmoja), vikundi vya wakulima na wakulima wakubwa yameongezeka katika maeneo makuu yafuatayo:

Eneo linalolimwa mazao ya biashara limeongezeka kutoka hekta 92,434 mwaka 2005 hadi hekta 115, 543 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 20.

Uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula umeongezeka hadi tani 968,654 kwa mwaka; sawa na ongezeko la asilimia 41 ikilinganishwa na kipindi cha nyuma. Kiasi hiki kinatosheleza mahitaji ya chakula kwa mkoa ambao mahitaji yake ni tani 894, 200. Hali hii ya uzalishaji chakula inatutoa katika kumbukumbu za kihistoria za njaa katika mkoa

wa mwanza za *Mapindasungwa* (yaani kejeli ya kisukuma kwa waliopewa msaada wa njaa wa mpunga na wakapika bila kukoboa wakiwa hawajawahi ona huo mpunga wa aina hiyo), njaa ya *legulegu( kipimo cha Mizani)*, njaa ya *magopo* (kwa maana watu walipatiwa chakula kwa vipimo vya makopo kama kipimo kikuu).

Uzalishaji wa mazao mbalimbali ya biashara umeongezeka hadi kufikia tani 99,360 kwa mwaka ; sawa na ongezeko la asilimia 92. Mbali na mazao ya asili ya biashara ya pamba yanayolimwa sasa yameongezeka mazao ya dengu na choroko kama mazao ya biashara.

Matumizi ya mbolea ya viwandani yameongezeka kutoka tani 640 mwaka 2005 hadi tani 7074 mwaka 2010, hali hiyo ni ongezeko kubwa ikilinganishwa ilivyokuwa mwaka 1961.

Matumizi ya mbolea ya samadi yameongezeka kutoka tani 560,000 (2005) hadi 700,000 (2010) tofauti na huko nyuma miaka ya 1961. Mbolea ya ruzuku imeongezeka kutoka tani 460 mwaka 2005 hadi tani 3411 mwaka 2010. Matumizi ya dawa ya pamba ya ruzuku imeongezeka kutoka pack 0 mwaka 2005 hadi acre pack 432,551 mwaka 2010. Mbegu ya pamba yaruzuku imeongezeka toka tani 0 mwaka 2005 hadi tani 2883 mwaka 2010.
Matumizi ya wanyamakazi maksai katika kilimo yameongezeka kutoka asilimia 25 mwaka 2005 hadi 32 mwaka 2010. Matumizi ya mbegu bora (mahindi , mtama na muhogo) yameongezeka kutoka tani 2806 mwaka 2005 hadi tani 4176 mwaka 2010.

Kupitia Halmashauri zetu, mkoa umejiwekea mikakati ya kuendesha kilimo kwa kutumia matrekta madogo. Kwamba, mkulima anaweza kutumia matrekta hayo kwa kupokezana kwa zamu na wakulima wenzake katika eneo lao kwa kuwa trekta lina uwezo wa kulima ekari nyingi zaidi kwa haraka ikilinganishwa na jembe la mkono. Takwimu za matrekta yaliyopo mkoani mwanza zinaonyesha, matumizi ya matrekta madogo yameongezeka kutoka 12 mwaka 2005 hadi 144 mwaka 2010. Yanategemewa kufikia 470 mwaka

2015. Matumizi ya matrekta makubwa yameongezeka kutoka 134 mwaka 2005 hadi 187 mwaka 2010. Yanategemewa kufika 388 mwaka 2015.

Pamoja na mkoa wetu kutegemea zaidi kilimo cha mvua za vuli na masika, katika mageuzi ya kilimo yaliyoanza miaka 50 iliyopita hadi leo hii, Kilimo cha umwagiliaji kimeongezeka kutoka hekta 1,173 mwaka 2005 hadi hekta 3532 mwaka 2010. Mategemeo ni kufikia hekta 10,000 mwaka 2015. Mafanikio makubwa yaliyopo mkoani mwanza ni pamoja na kujengwa kwa chuo kikubwa cha utafiti wa kilimo cha kanda cha Ukiriguru ambako kunazalishwa mbegu bora za mazao ya chakula na biashara.

Changamoto mbalimbali zinazoukabili mkoa katika masuala ya kilimo ni ;

- Kilimo hutegemea mvua kwa zaidi ya asilimia 90. Mvua haziaminiki na kiasi cha mvua kinachonyesha kimekuwa kikipungua mwaka hadi mwaka.
- Kilimo hutumia nyenzo duni yaani jembe la mkono hivyo kushindwa kurahisisha na kuharakisha shughuli za kilimo.
- Bei kubwa ya pembejeo za kilimo na hazipatikani kwa wingi katika maeneo ya vijijini na pia huchelewa kufika kwa wakati.
- Bei ndogo ya mazao ya kilimo inayosababishwa na msongomano /wingi wa mazao wakati wa mavuno na kufanya bei kushuka
- Wakulima kutozingatia kanuni za kilimo bora ikiwemo matumizi ya mbegu bora, viatilifu, mbolea na upandaji wa kuzingatia nafasi.
- Usimamizi hafifu wa wataalamu wa kilimo

### 4.3 MIFUGO

Mafanikio ya wakulima na wafugaji hayawezi kutenganishwa. katika mkoa wa Mwanza sekta ya mifugo katika miongo mitano iliyopita imepiga hatua kubwa kwa kuboreshwa maisha ya mifugo na wafugaji. Mwaka 1961, hali ya mifugo mkoani Mwanza ilikuwa ya mifugo mingi sana kwa kuwa maeneo ya malisho pia yalikuwa makubwa yasiyo na mipaka. Itakumbukwa kuwa dhana ya kupiga chapa ngombe ilianza wakati huo ili

kisheria ng'ombe wote wenye chapa lazima wafikishwe kuuzwa mnadani kwa lengo la kupunguza mifugo. Hali hii ilipelekea wafugaji wa kabila la Kisukuma kuwa wahamaji kutafuta malisho katika maeneo mbalimbali nchini.

Maendeleo yaliyofikiwa sasa ni mkoa una ng'ombe 1,654,726, ng'ombe wa maziwa 27,068, mbuzi wa kienyeji 770,354, mbuzi wa maziwa 659, kondoo 264,704 na nyati maji 80. Mkoa una huduma za mifugo kama ifuatavyo; eneo la malisho hekta 599,230 majosho yanayofanya kazi hadi kufikia 120 katika 189 mwaka 2010, vituo vya mifugo 33, vibanio 60, mabwawa makubwa 113, mabwawa madogo 361, machinjio makubwa 11, machinjio madogo 49 na minada 16. Watalaamu wa uhamilishaji (Artificial Insemination) wameongezeka hadi kufikia 34 mwaka 2010. Dawa za kuogesha mifugo zenye ruzuku ya serikali zimeongezeka kutoka lita 1,750 mwaka 2005 hadi lita 59,154 mwaka 2010. Thamani ya dawa hizo ni Tshs. 2.4bn/- Mashamba darasa ya ufugaji yamemeongezeka kutoka 0 mwaka 2005 hadi 3,807 mwaka 2010. Wafugaji waliopata mafunzo ya ufugaji bora katika mkoa hadi sasa ni 8,489.



*Sehemu ya kunyweshea mifugo katika lambo la kijiji cha Sogoso Sengerema mkoani Mwanza*

Vifo vya ndama kabla ya kufikia mwaka mmoja kutokana na magonjwa yaenezwayo na kupe vimepungua hadi **30%** kufikia mwaka huu 2011.

## 4.4 UVUVI

Mkoa wa Mwanza umebarikiwa kuwa na eneo la maji ya Ziwa Victoria lenye ukubwa wa kilometa za mraba 15,092 sawa na asilimia 43 ya eneo lote la mkoa. Aina ya samaki waliomo katika ziwa ni sangara, sato, hongwe, furu, mumi, kamongo, ningu, gogogo, nembe, kambalemamba na dagaa. Aidha kuna wanyama aina ya kiboko, mamba, kenge, nyoka wa majini, korongo na ndege wa aina mbalimbali. Uvuvi kabla ya Uhuru ulikuwa unafanyika kwa matumizi tu ya kawaida, kwa upande wa Biashara ilikuwa ni kidogo sana, kipato cha Mvuvi kilikuwa ni kidogo sana kwa sababu ya Zana duni walizokuwa wakitumia kama vile:- Magome ya miti yalitumika kama Mitumbwi wakati mapingili ya miti na kamba za katani zilishonea nyavu (Wavu). Kabla ya Uhuru Sekta ya Uvuvi ilisimamiwa na Serikali kwa njia ya Fisheries Ordinance Cap. 295 sheria ndogo hiyo ilirekebishwa miaka baada ya Uhuru. Miaka tisa baada ya Uhuru ilitungwa sheria ya Uvuvi Na. 6 ya 1970, sheria hii ilimpa nguvu Ofisa Uvuvi kuwa yeye ndiye msimamizi tu wa sheria hiyo. Mwaka 1997 iliundwa Sera ya Uvuvi iliyohusisha jamii kusimamia Rasilimali ya Uvuvi kwa kushirikiana na serikali. Mwaka 1999 – 2000 ziliundwa BMU (Beach Management Unit) katika Mialo kwa maana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi.

kipindi cha miaka 50 ya Uhuru kumekuwepo ongezeko la kuridhisha la shughuli za uvuvi. Mkoa mathalani mwaka 2006 ulikuwa na wavuvi 56,321, mitumbwi 16,911, nyavu 208,079, nyavu maalum za dagaa 3,455 na ndoano 2,264,792. Uvuvi hufanyika kwa matumizi ya injini za kupachika kwenye Mitumbwi na matumizi ya tanga. Injini zimeongezeka hadi kufikia 4,168 ikilinganishwa na hali ya mwaka 1961, matanga kutoka 348 hadi 1114 . Matumizi ya nyenzo hizi yanawawezesha Wavuvi kuvua kwenye maeneo ambayo yako mbali na fukwe za Ziwa.

Samaki aina ya sangara huvuliwa kwa wingi na kuuzwa kwenye masoko ya ndani na kwenye viwanda vya kuchakata minofu. Mwaka 2011 mkoa una viwanda vikubwa vya VicFish, Omega, Tanperch, Nile Perch, na TFDC. Samaki hao pia huuzwa nje ya nchi. Dagaa huvuliwa kwa wingi na kuuzwa ndani na nje ya Nchi hususani nchi za Maziwa Makuu.




*Soko la kisasa la kupokelea mazao ya Samaki toka ziwa Victoria lililopo kata ya kirumba jijini Mwanza*

Kumekuwepo na dhana kwamba samaki wamepungua katika ziwa victoria kutokana na kuongezeka kwa uvuvi wa kutumia dhana haramu kama sumu, timba na makokoro. Mkoa umechukua hatua ya kuwaelimisha wavuvi juu ya uvuvi endelevu ili kulinda na

kuhifadhi rasilimali ya ziwa. Jumla ya Wavuvi waliopewa elimu hii katika mkoa ni 7,798. Elimu hiyo itawasaidia kuhakikisha kuwa mapambano dhidi ya uvuvi haramu. Pia, mkoa umesimamia uanzishwaji wa BMU katika kila mialo.



*Uvunaji samaki mwalo wa Nkome Geita Mkoani Mwanza*

## 4.5 USHIRIKA

Mkoa wa Mwanza unajivunia miaka 50 ya uhuru kwa sababu historia ya ushirika na vyama vya ushirika ilianzia hapo. Mkoa hadi kufikia 2011 Sekta ya Ushirika imetekeleza yafuatayo:-

Idadi ya vyama vya Ushirika vya Akiba na mikopo (SACCOS) vimeongezeka kutoka vyama 245 mwaka 2005 hadi 646. Katika kipindi hiki SACCOS zimepata jumla ya mikopo yenye thamani ya Tshs.16, 219,676,630.15. Asilimia 91 imerejeshwa.

Chama kikuu cha ushirika katika mkoa wa mwanza ni NCU (1984) LTD, ambacho kihistoria kipo katika jengo la lilipokuwa shirikisho la kwanza la ushirika la Victoria.

### 4.6 ELIMU

Mfumo wa Elimu Tanzania umepita katika hatua mbalimbali kama vile, Elimu kabla ya ukoloni, Elimu wakati wa Ukoloni, Elimu baada ya uhuru, Elimu baada ya Azimio la Arusha (1978), kuundwa kwa Tume ya Rais mwaka 1981 kuhusu Elimu, kuwepo kwa 'Task force" kuhusu Elimu 1990 na Mfumo wa Elimu katika karne ya 21.

Mkoa wa Mwanza kufikia mwaka 2011 una jumla ya shule za Awali 787, msingi 1219 kati ya hizo za serikali ni 1167 na za binafsi 52. Shule hizi zina takribani jumla ya wanafunzi 853,459 ambapo wavulana 426,095 na wasichana 427,364. Mkoa una jumla ya walimu 15165. Mahitaji ya walimu ni 20851 na upungufu ni 5686 sawa na asilimia 27.3. Mkoa wa Mwanza una madarasa 9270 wakati mahitaji ni 20090 na upungufu ni 10820**,** Nyumba za walimu zilizopo ni 2874, mahitaji yakiwa ni 19145 na upungufu ni nyumba 16271. Matundu ya vyoo yaliyopo ni 10995 wakati mahitaji ni matundu 38831 na upungufu ni 27836.

Shule za sekondari zilizokuwepo wakati wa uhuru ni Bwiru wavulana (1920), Bwiru Wasichana (1952), Mwanza (Chopra) (1959) na Nsumba (Rozary) (1953). Mwaka 2011 Mkoa wa Mwanza una jumla ya shule za Sekondari 292 kati shule hizo, za Serikali ni 237 na zisizo za serikali ni 55. Kati ya shule hizo shule 14 za serikali na shule 16 za binafsi zina kidato cha V na VI

Idadi ya Shule za Sekondari zilizopo mkoani Mwanza

| **WILAYA** | **SERIKALI** | **ZISIZO ZA SERIKALI** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| GEITA | 44 | 2 | 46 |
| ILEMELA | 23 | 19 | 42 |
| KWIMBA | 27 | 1 | 28 |
| MAGU | 33 | 4 | 37 |
| MISSUNGWI | 22 | 5 | 27 |
| NYAMAGANA | 28 | 14 | 42 |
| SENGEREMA | 39 | 8 | 47 |
| UKEREWE | 21 | 2 | 23 |
| **JUMLA** | **237** | **55** | **292** |

Shule za Sekondari zenye Kidato cha V – VI 2011

| **WILAYA** | **SERIKALI** | **ZISIZO ZA SERIKALI** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| GEITA | 2 | 1 | 3 |
| ILEMELA | 2 | 7 | 9 |
| KWIMBA | 3 | 0 | 3 |
| MAGU | 1 | 0 | 1 |
| MISSUNGWI | 0 | 2 | 2 |
| NYAMAGANA | 5 | 4 | 9 |
| SENGEREMA | 1 | 2 | 3 |
| UKEREWE | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA** | **14** | **16** | **30** |

Walimu katika Shule za Sekondari:
Mkoa wa Mwanza wenye jumla ya shule za sekondari za serikali 237 ina jumla ya walimu 3175 na mahitaji ya walimu ni 5894 na upungufu ni 2719 sawa na asilimia 46.2%.

Idadi ya walimu katika mkoa

| **WILAYA** | **MAHITAJI** | **WALIOPO** | **UPUNGUFU** |
|---|---|---|---|
| GEITA | 1318 | 357 | 961 |
| ILEMELA | 613 | 451 | 162 |
| KWIMBA | 801 | 528 | 273 |
| MAGU | 818 | 452 | 366 |
| MISSUNGWI | 305 | 141 | 164 |
| NYAMAGANA | 916 | 655 | 261 |
| SENGEREMA | 673 | 415 | 258 |
| UKEREWE | 450 | 176 | 274 |
| **JUMLA** | **5894** | **3175** | **2719** |



*Jengo la zamani la Shule ya Msingi Sengerema lililotumika kama Lower Primary School (darasa la I – IV).*



*Nyumba za walimu shule ya sekondari Bukandwa Ukerewe mkoani Mwanza*

Elimu ya juu

Mkoa wa Mwanza una vyuo vya elimu ya juu vya CBE, SAUT, OUT,ADEM, Chuo Kikuu cha Tiba na Afya cha Bugando na Mzumbe University ambavyo vimefunguliwa kukidhi mahitaji ya elimu ya juu.



*Jengo la Chuo Kikuu cha SAUT jijini Mwanza*

## 4.7 AFYA

Huduma za afya katika mkoa wa Mwanza zinatolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando, Hospitali ya Mkoa ya Sekou Toure, Hospitali nyingine 13 zikiwemo 6 za Wilaya, vituo vya afya 45 na zahanati 340. Magonjwa yanayowasumbua wakazi wa Mkoa huu ni pamoja na malaria, magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya hewa na VVU/UKIMWI.

Mlinganisho wa huduma za afya 1961-2011

| **Wilaya** | **zahanati** | | **Vituo vya afya** | | **hospitali** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 |
| Geita | 7 | 52 | 0 | 9 | 1 | 1 |
| Sengerema | 2 | 55 | 0 | 8 | 0 | 1 |
| Ilemela | 0 | 38 | 0 | 5 | 0 | 1 |
| Nyamagana | 1 | 38 | 0 | 7 | 1 | 6 |
| Kwimba | 0 | 32 | 0 | 5 | 0 | 2 |
| Magu | 0 | 61 | 0 | 6 | 0 | 2 |
| Misungwi | 0 | 32 | 0 | 4 | 0 | 2 |
| Ukerewe | 4 | 32 | 0 | 1 | 1 | 1 |
| **JUMLA** | **14** | **340** | **0** | **45** | **3** | **16** |

Maambukizi ya malaria katika Mkoa wa Mwanza ni asilimia 31.4%. jitihada zinafanyika katika kupambana na ugonjwa wa malaria Mkoani za utoaji wa vyandarua kwa watoto na akina mama wajawazito kupitia mpango wa hati punguzo. Hadi kufikia Novemba, 2010 vyandarua vya hati punguzo 724,697 zimekwishatolewa kadhalika upuliziaji wa dawa ya ukoko katika Kaya za Halmashauri za Kwimba, Magu na Missungwi ulifanyika, ambapo Kaya 506,209 zimenyunyiziwa dawa sawa na 92% ya matarajio.

Maambukizi ya UKIMWI katika Mkoa wa Mwanza ni asilimia 5.6%, Hadi kufikia mwezi Septemba 2010 watu 53,644 wamesajiliwa katika vituo 57 vya kutolea huduma na matibabu ya UKIMWI Mkoani. Kati yao 25, 135 sawa na 47% wanatumia dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI.

Mkoa katika kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI unatoa elimu ya afya ; kuhamasisha upimaji wa hiari wa VVU ; huduma na matibabu kwa wagonjwa vituoni na majumbani ; unadhibiti magonjwa ya zinaa na kifua kikuu na kuhamashisha matumizi ya mipira ya kondomu kwa wale wanaoshindwa kufuata njia zingine za kinga.

## 4.8 MIUNDOMBINU

Miundo mbinu iliyopo mkoani mwanza tangu uhuru ni ile ya reli ya kati iliyojengwa na wajerumani mwaka 1918 kwa lengo la kusafirisha malighafi, mabarabara, bandari na viwanja vya ndege. Aidha, kumekuwepo mabadiliko mbalimbali ya miundombinu hii kwa kipindi cha miaka 50 tangu uhuru. Mafanikio ya miaka 50 ya Uhuru ya Miundombinu imejikita katika maeneo yafuatayo:-

### 4.8.1 Mtandao wa barabara Mkoa wa Mwanza 1961

Tangu kupata Uhuru 1961, mtandao wa barabara umeimarika kwa kujenga barabara mpya za lami na barabara za changarawe, na kufungua barabara mpya za udongo mkoani ili kuimarisha na kurahisisha mawasiliano. Pia halmashauri zimeweza kuongeza mtandao wa barabara kati ya wilaya na vijiji vyake kurahisisha mawasiliano.

Mtandao wa barabara mkoa wa Mwanza mwaka 1961

| **Aina ya Barabara** | **Lami (km)** | **Changarawe (km)** | **Udongo (km)** | **Jumla (km)** |
|---|---|---|---|---|
| Barabara kuu | 0 | 0 | 394.35 | 394.35 |
| Barabara za Mkoa | 0 | 0 | 773.94 | 773.94 |
| Barabara za Wilaya | 8.81 | 125 | 1165 | 1298.81 |
| Barabara za Vijiji | 0 | 0 | 255.5 | 255.50 |
| **Jumla** | **8.81** | **125** | **2588.79** | **2722.60** |

Mwaka 1961, mkoa wa Mwanza haukuwa na barabara kuu za lami wala changarawe. Kulikuwa na barabara za udongo zenye urefu wa km 394.35. Kwa upande wa barabara za mkoa kulikuwa na barabara za udongo za urefu wa km 773.94. Barabara za wilaya lami ilikuwa na urefu wa km 8.81, changarawe km 125 na udongo ni km 1165, na barabara za vijiji zilikuwa za udongo urefu wa km 225.5.

## Mtandao wa barabara mkoa wa Mwanza baada ya uhuru hadi 2011

Baada ya Uhuru, serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kuunganisha barabara kati ya vijiji na barabara za wilaya, mikoa na barabara kuu ili kurahisisha mawasiliano na kuinua uchumi wa wananchi. Serikali imeendelea kuimarisha na kuongeza ujenzi wa mtandao wa barabara kwa kujenga barabara za lami, changarawe na udondo. Hivi sasa, mkoa una jumla ya barabara kuu za lami zenye urefu wa km 376.31 na barabara za changarawe za urefu wa km 33.52. Barabara za mkoa zenye lami ni km 16.63 na barabara za changarawe km 1107.18. Pia barabara za wilaya zenye lami ni km 31.20, changarawe km 1295.82 na udongo km 3008.23. Barabara za vijiji za changarawe ni km 156.90 na udongo km 2039.48.

Mtandao wa barabara mkoa wa Mwanza hadi mwaka 2011

| **Aina ya Barabara** | **Lami (km)** | **Changarawe (km)** | **Udongo (km)** | **Jumla (km)** |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Barabara kuu | 376.31 | 33.52 | 0 | 409.83 |
| Barabara za Mkoa | 16.63 | 1107.18 | 0 | 1123.81 |
| Barabara za Wilaya | 31.20 | 1295.82 | 3008.23 | 4335.25 |
| Barabara za Vijiji | 0 | 156.90 | 2039.48 | 2196.38 |
| **Jumla** | **424.14** | **2593.42** | **5047.71** | **8065.27** |

Mafanikio:

mafanikio ya miaka 50 ya uhuru sekta ya barabara ni kama ifuatavyo:-

- Barabara kuu za lami ambazo hazikuwepo zimejengwa zenye urefu wa km. 376.31
- Barabara kuu za changarawe ambazo hazikuwepo zimejengwa zenye urefu wa km. 33.52
- Barabara za mkoa za lami ambazo hazikuwepo kabisa zimejengwa zenye urefu wa km. 16.63
- Barabara za mkoa za changarawe ambazo hazikuwepo zimejengwa zenye urefu wa km. 376.31
- Barabara za wilaya za lami zimeongezeka kutoka km 8.81 hadi km 31.20 sawa na asilimia 254.
- Barabara za wilaya za changarawe zimeongezeka kutoka km 125 hadi km 1295.82 sawa na asilimia 936.
- Barabara za wilaya za udongo zimeongezeka kutoka km 1165 hadi km 3008.23 sawa na asilimia 158.2.
- Barabara za vijiji za udongo zimeongezeka kutoka km 255.5 hadi km 2039.48 sawa na asilimia 698.2.

### 4.8.2 Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Ukuaji wa Miji

Mkoa una wilaya nane (8) na halmashauri saba (7) tarafa 33 kata 214 na vijiji 701. Makao makuu ya halmashauri hizi yako kwenye Jiji la Mwanza na miji midogo ya wilaya. Halmashauri tano (5) kati ya saba (7) katika mkoa wetu tayari zimeanzisha mamlaka ya miji na miji midogo. Halmashauri hizo ni Jiji, Sengerema, Magu, Kwimba na Ukerewe.



*Utekelezaji wa mipango miji na uwekezaji mkoani Mwanza*

Mji wa Mwanza

Mji wa Mwanza ulianzishwa mwaka 1892 ukiwa ni Makao makuu ya utawala na biashara katika mkoa wa Mwanza. Mji huu uliendelea kukua kwa haraka kwa 11% . Watu walikuwa katika mji wa Mwanza kama ifuatavyo; 11,300 (1948), 19,900 (1957), 169,660 (1978), 223,013 (1988), 476,642 (2002). Kufikia mwaka 2011 mji unakadiriwa kuwa na watu 750,000. Mwaka 1978 mji ulipata hadhi ya kuwa Manispaa na ilipofikia mwaka 2000 uliteuliwa kuwa Jiji. Huu ni mji wa pili kwa ukubwa nchini Tanzania ukiwa na eneo la kilomita za mraba 1,325 ambapo kilomita za mraba 900 ziko ndani ya maji na kilomita za mraba zilibakia 425 ziko nchi kavu.

Mji unakadiriwa kuwa na nyumba 70,000. Nyumba zipatazo 51,000 kwenye maeneo yasiyopimwa kiasi ambacho ni asilimia 73% ya nyumba zote za Jiji. Inasadikiwa kwamba 70% ya watu walioko jijini Mwanza wanaishi kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Mipango ya matumizi bora iliyofanyika:

- Mpango kamambe wa Jiji la Mwanza 1992 – 2012 (master plan)
- Mpango wa uendelezaji mjini kati (Central Area Redevelopment Plan 1993 – 2013)
- Kuboresha makazi yasiyo rasmi (upgrading) 1998
- Kuorodhesha mali za kudumu (formalization of properties)
- sustainable city program under DANIDA 2001
- Kupima na kutoa huduma kwa viwanja vipya 10,000
- Mradi wa urasimishaji wa makazi.

Miji iliyoidhinishwa kuwa miji midogo kwenye halmashauri ni kama ifuatavyo:-

- Halmashauri ya wilaya ya Magu

  Mji mdogo wa Kisesa, Lamadi, Nyanguge, Nyamikoma, Nassa, Kabila, Kayenze Masanzakona na Mkula.
- Halmashauri ya wilaya ya Misungwi

  Mji mdogo wa Usagara, Misasi, Mabuki Kigongo Ferry na Seke.
- Halmashauri ya wilaya ya Kwimba.

  Mji mdogo wa Malya, Nyambiti Sumve, Hungumalwa.
- Halmashauri ya wilaya ya Ukerewe

  Mji mdogo wa Mriti, Murutunguru, Bwisya na Rugezi.
- Halmashauri ya wilaya ya Sengerema

  Mji mdogo wa Nyehunge, Kamanga Busisi, Bupandwa, Katunguru, Kahunda na Ngoma.
- Halmashauri ya wilaya ya Geita

  Mji mdogo wa Kasamwa, Bukoli, Katoro, Nyarugusu Nkome na Karumwa.

Upimaji wa vijiji

Katika Mkoa wa Mwanza utaratibu wa uhamasishaji na upimaji vijiji ulianzia mwaka 1996. Kufikia mwaka huu 2011 utekelezaji umekuwa kama ifuatavyo:-

| S/Na. | Wilaya | Idadi ya Vijiji | Vijiji vilivyopimwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Magu | 124 | 13 | 10 |
| 2. | Misungwi | 78 | 58 | 74 |
| 3. | Kwimba | 111 | 31 | 28 |
| 4. | Sengerema | 123 | 20 | 16 |
| 5. | Geita | 197 | 143 | 73 |
| 6. | Ukerewe | 68 | 15 | 22 |
| **Jumla** | | **701** | **280** | **40** |

Urasimishaji wa Makazi holela

Wizara ya ardhi na Maendeleo ya Makazi katika utekelezaji wa sheria ya ardhi ya mwaka 1999 inasimamia na kutekeleza miradi ya urasimishaji wa makazi yaliyojengwa kiholela nchini kuanzia mwaka 2004/2005; kwa kutekeleza sheria hiyo Wizara imeanzia na Jiji la Dar es Salaam kwa kutoa leseni za makazi ili kuongeza usalama wa miliki na kuelekeza kutoa hati miliki kwa jiji la Mwanza kwa kuzingatia kifungu (56 – 60) kama maeneo ya majaribio.Mwaka 2006 utekezaji wa mpango huu uliingiwa kwenye programu ya kuboresha ushindani katika sekta binafsi katika kuboresha sekta ya ardhi, inayofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya ofisi ya Waziri Mkuu. Miradi ya urasimishaji inaendelea kutekelezwa na halmashauri za mji iliyobakia kote nchini kama mojawapo ya majukumu yaliyoelekezwa katika sheria ya ardhi na ile ya mipangomiji ya mwaka 2007.

Mradi wa urasimishaji ulianza tarehe 1.4.2009 kwa kata kumi zilizoko jijini Mwanza ambazo ni kata ya Buhongwa, Nyakato, Mahina, Mkolani, Kitangiri, Butimba, Pasiansi, Kirumba, Isamilo na Igoma. Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mradi ni Tshs. 1.6 Bilioni. Hadi kufikia Juni, 2011 Tshs. Milioni 791,512,140/= zilikuwa zimepokelewa na kwamba Tshs. 775,512,140 tayari zimetumika. Aidha kazi zilizofanyika ni utambuzi wa miliki 33,627, uaandaji wa michoro ya mipangomji yeye viwanja 20,391 na upimaji wa viwanja 9.042. Tayari hati 1,382 zimeandaliwa na kupewa wananchi. Kwa mujibu wa taarifa ya mradi kazi zilizofanyika zinafikia asilimia 69%. Mradi umekumbwa na

changamoto nyingi ikiwepo migogoro ya mipaka ya ardhi, msongamano wa nyumba na maeneo mengi kuwa milimani.

Msajili wa Hati

Ofisi ya Msajili wa Hati ilianzishwa wakati wa utawala wa Kijerumani mnamo mwaka 1891. Utawala wa Kiingereza ulipochukuwa mamlaka masuala ya usajili wa hati yaliendelea kwa maana ya kutambua milki zingine. Wakati huo ofisi ya Msajili wa Hati ilikuwa nchini ya Kabidhi Wasii katika Wizara ya Sheria mpaka mwaka 1965 ilipohamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama kitengo kamilli kinachojitegemea.

Mnamo mwaka 1972 Idara ya Usajili ilihamia chini ya Idara ya Ardhi kuwa sehemu katika Idara hiyo kwa lengo la kupunguza matumizi. Mnamo mwaka 2007/2008 kutokana na majukumu ya kazi yaliyopo na mwamko wa wananchi na wawekezaji kuhusu masuala ya Ardhi, serikali iliona umuhimu wa kuifanya sehemu ya Usajili wa Hati kuwa kitengo kamili kinachojitegemea katika masuala ya bajeti na kiutendaji.

Mafanikio 1961 - 2011:

Baada ya Serikali kuanzisha ofisi za Kanda ikiwemo hii ya Mwanza wananchi wengi wamekuwa wakisajiliwa hati zao na kuweza kuzitumia katika kufanya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tangu ofisi hii ilipoanzishwa imeweza kusajili hati miliki 43,000.

(a) Sheria zilizopitishwa kuboresha Usajili wa Hati: 1999 – Sheria ya Ardhi ya Vijiji (The Village Land Act No. 5/1999) Kwa kutambua umuhimu wa ardhi kwa wananchi walio wengi serikali imepitisha sheria hii pamoja na mambo mengine imewezesha uanzishaji wa Masjala za Ardhi za Vijiji nchini.

Kwa kuzingatia sheria hii Vijiji vinaweza kupatiwa vyeti ambavyo vinaonyesha eneo linalomilikiwa na kijiji husika na hatimaye miliki ardhi za kimila (certificate of Customary Right of Occupancy).

(b). 2008 – Sheria ya Umiliki wa sehemu ya jengo (Unit Title Act.  Na. 17/2008)
Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo ilipitishwa ili kuwezesha wamiliki wa sehemu ya jengo kuweza kumiliki maeneo yao na kupata hati miliki ambazo wanaweza kuzitumia na kupata manufaa aidha kwa kuzitumia kama dhamana au kujihakikishia uhalali wa maeneo wanayomiliki (Security of Tenure).

(c) 2008 – Mortgage Financing (Special Provisions) Act Na. 18/2008.
Sheria hii imewezesha kuondoa kikwazo cha upatikanaji wa vibali kutoka ofisi ya Kamishna wa Ardhi ili kuweka dhamana hati miliki katika taasisi za fedha. Sheria hii imeondoa hitajila kibali na imewezesha usajili wa rehani kufanyika kwa ufanisi zaidi hivyo kuondoa urasimu uliokuwepo hapo awali. Upimaji wa maeneo na utoaji wa hati za kumiliki ardhi huwezesha serikali kuwa na kumbukumbu zinazoweza kutumika kwa ajili ya kupata mapato ya serikali. Mfano kodi za ardhi na mapato mbalimbali yanayopatikana kutokana na ada mbalimbali zinazotokana na mamala katika ardhi.

**4.8.3 Reli:**
Usafiri wa reli uliendelea kuimarishwa baada ya uhuru kwa kukarabatiwa kwa reli ya kati kutokea Dar es salaam hadi Mwanza. Usafirshaji wa abiria na mizigo uliongezeka baada ya serikali kuunda shirika la Reli Tanzania wakati huo(TRC) lililounganisha mawasiliano na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na nchi jirani za maziwa makuu kupitia bandari ya Mwanza North na Mwanza South. Meli za MV Victoria ni matunda ya meli zilizojengwa mwaka 1961 mara baada ya uhuru na imekuwa ikifanyiwa marekebisho kulingana na taratibu za usalama wa vyombo vya majini na kubwa zaidi mwaka 2007 ilifanyiwa ukarabati ulioirudisha katika hali ya upya kwa asilimia 90. TRC baada ya ubinafsishaji kuwa TRL imekumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uharibifu wa miundombinu ya reli.

Matarajio ya serikali ni kuendelea kuboresha sekta hiyo kwa kuisaidia TRL kwa ubia kuipatia mabehewa na menejimenti itakayoendesha shirika hilo vizuri zaidi.

Kumekuwepo huduma bora za usafiri wa majini na ongezeko la vyombo vya usafiri vya watu binafsi katika ziwa Victoria. Mfano usafiri wa meli za kwenda ukerewe meli mpya za watu binafsi za mizigo na abiria zimeweza kufanya safari za uhakika na kuwezesha maeneo haya kufikika kwa urahisi. Meli za mwanzo baada ya uhuru zilizokuwepo nazo zimeendeelea kuimarishwa kimatengenezo na kuboresha huduma zaidi hasa baada ya Kuanzishwa kwa Shirika la Huduma za Meli(MSL)na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari(TPA).

### 4.8.4 Vivuko:

Mkoa wa mwanza una vivuko na magati yanayohudumia mkoa katika maeneo ya usafirir wa majini ziwani na hali hii wakati wa uhuru ilikuwa ya kuridhisha ikilinganiwa na sasa hali kuwa nzuri sana katika maeneo ya Kigongo ferry, kamanga ferry, bugorola na rugezi. Serikali itandelea kuboresha vivuko vya maeneo yote ya visiwani ya nkome na nyakaliro ili kusaidia maeneo hayo kufikika kwa uhakika zaidi.




*Kivuko cha MV Misungwi kinachofanya safari kati ya Busisi – Kigongo mkoani Mwanza*

### 4.8.5 Viwanja vya ndege:

Huduma za viwanja vya ndege wakati wa uhuru ilikuwa ni ya kuridhisha. Hivi sasa mkoa wa mwanza una uwanja mkubwa na unaendelea kupanuliwa ili ufikie kiwango cha kimataifa. Uwanja wa sasa una uwezo wa kupokea na kupaki ndege kubwa zaidi ya 10 aina ya D 8 kwa wakati mmoja. Uwanja huu unahudumia usafirir wa abiria na pia mizigo mbalimbali ndani ya na nje ya nchi. Makampuni ya ndege sasa yameongezeka toka Air Tanzania baada ya Uhuru na sasa kuna Precision Air, Jetlink, Aviation Air, Coastal, Euric air, Fly 540, community Airline ambayo yanatoa huduma katika uwanja huo. Mkoa una uwanja wa ndege mkubwa Geita na vingine vidogo Rubondo, Ukerewe, na Sumve.

### 4.8.6 Mwasiliano ya simu

Mkoa wa mwanza wakati wa uhuru 1961hadi miaka ya 1980 mawasiliano ya simu hayakuwa ya kuridhisha sana. Wakati huo mawasiliano yalilazimika kufanyika kwa njia ya simu za upepo ili kuyafikia maeneo ya vijijini. Hali hii ilipelekea baadhi ya maeneo ya mkoa kubatizwa majina ya maeneo yenye mazingira magumu, hata watumishi waliopelekwa huko wengi waliacha kazi kwa hofu kuwa maeneo hayo yaliwafanya watengwe na jamaa zao au maendeleo ya ulimwengu. Hivi sasa maeneo yote ya mkoa wa mwanza yana mawasiliano ya simu tena ya kisasa. Mitandao ya makampuni binafsi na ya umma ya Vodacom, Airtel, Zantel, Tigo na TCCL yameboresha huduma za mawasiliano za ndani na nje ya nchi. Wananchi wa mkoa wa Mwanza wapatao asilimia 35 hivi sasa wanatumia mawasiliano ya simu na inategemewa kufikia mwaka 2015 itafikia asilimia 50 ya wananchi wote.



*Moja ya minara ya kampuni ya simu za mkononi katika eneo la mlima wa Mwalolela kijiji cha Busulwangiri sengerema mkoani Mwanza.*

**4.8.7 Nishati na Madini:**

Nishati ya umeme wa jua, umeme wa Tanesco, kuni, mkaa na gesi asilia nay a wanyama vimekuwa vikitumiwa na wananchi wa mwanza kwa muda mrefu mara baada ya uhuru. Hata hivyo, kuna ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya umeme wa Tanesco kwa maeneo yote ya mijini katika mkoa wa mwanza. Mwaka 1961, hapakuwepo na ummeme wa tanesco lakini hivi sasa wilaya zote zimeunganishwa nishati hiyo. Wilaya zilizounganishwa karibuni zaidi ni za ukerewe mwaka 2005, Geita mwaka 2000, sengerema 1998, Kwimba na Missungwi 1992. Kukua kwa haraka kwa mkoa wa Mwanza na maeneo yake mathalani mkoa mpya wa Geita sasa kumechangiwa kwa kiasi kubwa sana na uwepo wa nishati ya umeme na pia uchimbaji wa madini wa makampuni makubwa ya GGM. Shughuli za kandarasi za majenzi mkoani mwanza hususani geita zimekua kwa kasi kubwa kutokana na uwepo uchimaji wa makampuni makubwa. Uchumi wa watu binafsi na jamii ya wananchi wa mwanza umekua kwa kasi

kutokana na uchimbaji mdogo mdogo wa mashapo ya dhahabu, lakini pia kutokana na ongezeko la ajira katika makampuni yenye kandarasi kubwa mbalimbali mkoani.

Mpango wa maendeleo wa miaka mitano umelenga kupeleka nishati ya umeme zaidi katika maeneo ya vijijini kwa mradi unaotekelezwa wa mfuko wa milennia(MCC). Aidha, njia bora za uwekezaji mkubwa wenye tija katika maeneo ya migodi utausaida mkoa wa Mwanza kutumia fursa zake kuwekeza zaidi kwenye maeneo hayo ili kuwa na uchumi chanya kwa maendeleo yote ya kisekta. Changamoto kubwa inayokabili sekta ya madini nchini ikiwepo mwanza ni kutotambua kuwa uwekezaji mkubwa una tija kubwa katika kuleta matokeo ya haraka katika maendeleo ya kiuchumi kuliko sekta nyingine za uzalishaji. Mkoa wa mwanza unakazania zaidi uwekezaji mkubwa katika wilaya na jiji kwa kutambua kuwa hiyo ndiyo njia pekee itakayoleta matokeo ya haraka ya kupunguza umaskini na kukuza pato la mkoa, njia hiyo ndio imefikisha mkoa huu hapo ulipo hivyo halmashauri za wilaya na Jiji zitaendelea kuthubutu kutumia fursa hiyo.

## 4.9 MAJI

### 4.9.1 Maendeleo ya Huduma ya Maji

Huduma ya maendeleo ya maji imepata mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

- Idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka 3 mwaka 1961 hadi 13 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 333.3.
- Idadi ya malambo imeongezeka kutoka 36 mwaka 1961 hadi 72 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 100.
- Miradi ya maji ya bomba imeongezeka kutoka 6 mwaka 1961 hadi 60 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 900.
- Idadi ya chemichemi iliyoboreshwa imeongezeka kutoka 5 mwaka 1961 hadi 8 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 60.

- Idadi ya miradi ya visima vya asili ambayo imeboreshwa ambayo haikuwapo mwaka 1961 imeboreshwa 257 hadi ilipofika mwaka 2011.
- Idadi ya visima vya pampu (virefu na kati) ambavyo havikuwapo mwaka 1961, vimejengwa 2743 hadi ilipofika mwaka 2011.
- Idadi ya matenki ya kuvuna maji ya mvua ambayo hayakuwapo mwaka 1961, yamejengwa 178 hadi ilipofika mwaka 2011.

**Jedwali Na 3: Vyanzo vya Maji mkoa wa Mwanza kati ya mwaka 1961 - 2011**

| | **Wilaya** | **Ngudu** | | **Magu** | | **Misungwi** | | **Geita** | | **Sengerema** | | **Ukerewe** | | Jiji | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Chanzo cha maji | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 | 1961 | 2011 |
| 1 | Mabwawa | 2 | 0 | 0 | 4 | 0 | 3 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 13 |
| 2 | Malambo | 36 | 2 | 0 | 22 | 0 | | | 31 | 0 | 15 | | | 0 | 2 | 36 | 72 |
| 3 | Miradi ya Maji bomba | 4 | 8 | 1 | 12 | 0 | 8 | 1 | 8 | 0 | 10 | 0 | 11 | 0 | 3 | 6 | 60 |
| 4 | Chemichemi | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 8 |
| 5 | Visima vya asili vilivyoboreshwa | 0 | 40 | 0 | 67 | 0 | 1 | 0 | | 0 | 0 | | 148 | 0 | 1 | 0 | 257 |
| 6 | Visima vya pampu za mkono ( vifupi na Kati) | 0 | 729 | 0 | 777 | 0 | 331 | 0 | 300 | 0 | 298 | | 225 | 0 | 83 | 0 | 2,743 |
| 7 | Tank za kuvuna maji ya mvua | 0 | 55 | 0 | 54 | 0 | 14 | 0 | 18 | 0 | 17 | | 15 | 0 | 5 | 0 | 178 |
| | | 43 | 834 | 1 | 938 | 0 | 357 | 6 | 367 | 0 | 340 | 0 | 399 | 0 | 96 | 50 | 3,331 |

### 4.9.2 Mafanikio ya Huduma za Maji kwa miaka 50 ya Uhuru.

Huduma ya Maji katika Mkoa wa Mwanza imeweza kuboreshwa kupitia program na sera mbalimbali za maji katika kipindi chote tangu kupatikana uhuru hasa katika mambo yafuatayo**.**

- Hali ya utoaji wa huduma ya maji Mkoani Mwanza imeboreshwa na kufikia 64% ya wakazi wake kupata maji safi na salama ukilinganisha kabla ya uhuru ambapo asilimia 19 ya wanachi walipata maji safi na salama.
- Serikali imefanikisha uundaji wa Bodi za Mamlaka za Maji katika miji ya makao makuu ya Wilaya Sita nakuleta ufanisi katika utendaji wake ukilinganisha na kabla ya uhuru ambapo hazikuwepo.
- Serikali imejenga mradi mkubwa wa Maji unaoitwa KASHWASA katika chanzo cha Ihelele ambao ni mkubwa nchi nzima ambao haukuwapo wakati wa uhuru.
- Huduma ya maji mjini Mwanza imeboreshwa na kufikia 90% ya wakazi wake kupata maji safi na salama ukilinganisha na 35% kabla yauhuru.
- Idadi ya visima vya maji imefikia jumla ya 2986 katika Mkoa
- Serikali imeweza kupata Sheria mpya ya maji namba 10, 11 na 12 ya mwaka 2009 ambazo inazingatia utaji wa huduma za maji vijijini, mijini na usimamizi wa rasilimali za Maji ukilingalisha na iliyokuwa ya Mkoloni ya sheria ya Tanganyika ya mwaka 1947-1950, kifungu 281 ambacho kilizingatia utaji wa huduma ya maji kwa viongozi tu.

### 4.9.3 Changamoto

- Miradi mingi ya maji ya iliyojengwa miaka ya 70 hadi 90 ilikufa kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji na matengenezo ya miradi na hujuma za wizi wa miundombinu (mfano; miradi iliyojengwa kupitia mpango wa HESAWA na miradi ya bomba Vijijini).
- Ukuaji wa watu katika miji ni mkubwa ukilinganisha na rasimali za upanuzi wa huduma za maji Mijini, Miundombinu ya maji iliyojengwa haitoshelezi mahitaji ya watu kwa sasa husuani Mji wa Ngudu, Magu, Geita na Ukerewe.

- Ukosefu wa vifaa vya kufanyia matengezo ya mabomba kama magreda ya kunyanyulia mizigo hususani kwenye miradi ya Mamlaka za maji kubwa za KASHWASA na MWAUWASA.

### 4.9.4 **Mipango ya baadaye**.

- Serikali kuendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo Sekta ya maji ambayo serikali imelenga kuwapatia wanachi huduma ya maji vijijini na mijini kufikia asimia 90 kwa Vijijini na asilimia 100 mijini ifikapo mwaka 2025.

- Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira katika Miji ya Sengerema, Magu, Geita na Ukerewe kwa ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika mashariki kuanzia mwaka 2013 hadi 2025.

- Serikali kuendelea kushirikiana na wafadhili mbalimbali na mashirika binafsi katika kuboresha huduma ya maji mijini na vijijini kupitia miradi tengefu (earmark project) ikiwa ni pamoja na ile inayofadhiliwa na JICA Phase II kuanzia mwaka 2013 na mradi wa maji Geita Mjini kwa ushirikiano wa G.G.M kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012.

## 4.10. VIVUTIO VYA UTALII NA FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA MKOA WA MWANZA

Biashara

Mkoa unavyo viwanda vikubwa na vya kati 42 ambavyo vinazalisha soda, bia, maji, magodoro, samaki, nguo, nondo, mafuta ya kupikia, n.k., Viwanda vidogo viko 30 ambavyo hujishughulisha na kuzalisha vinywaji, kuchonga vyuma, kusaga vyakula, kutengeneza samani, misumari n.k.. Viwanda vidogo vidogo viko 372 ambavyo hujishughulisha na kushona viatu, kushona nguo, kutengeneza mabegi, kusindika vyakula n.k.

Hali ya uwekezaji na fursa za uwekezaji zilizopo**:**

Sera ya Uwekezaji ilianza kutiliwa mkazo mkoani Mwanza kuanzia mwaka 2004 wakati uongozi wa Mkoa ulipofanya Kongamano la Uwekezaji (Mwanza Investors' Forum). Lengo lilikuwa ni kuhakikisha Mkoa unatenga maeneo ya kutosha ya uwezekazaji. Nia na madhumuni ya kuvutia uwekezaji ni kuinua uchumi wa Mkoa kwa kuongeza viwanda na ajira kwa wananchi wake. Katika kuendeleza mikakati ya kuvutia wawekezaji na kuweka mazingira shindanishi mkoa ulishiriki katika kongamano la kwanza la uwekezaji katika bonde la ziwa Victoria (Lake Victoria Basin Investment Forum) katika hoteli ya Malaika tarehe 05-08 Desemba 2010. Kongamano hilo la kihistoria lengo lake kuu lilikuwa kujadili utambuzi wa faida za uchumi na kijamii zinazotokana na uwekezaji katika bonde la ziwa Victoria.

Katika kuendeleza uwekezaji, mkoa unaendelea kufanya yafuatayo:

Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza ili uwe wa kimataifa na kuna mipango endelevu ya kuendeleza kiwanja hicho kwa awamu kuu tatu. Awamu ya kwanza ni mpango wa muda mfupi unaohusu ukarabati wa maegesho ya ndege za mizigo na abiria, ukarabati wa njia ya ndege, ujenzi wa maegesho ya magari, ujenzi wa jengo jipya la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni moja kwa mwaka, ujenzi wa jengo la kuhifadhia mizigo na urefushaji wa barabara ya kurukia na kutua mita 550 na ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege. Awamu ya pili ni utekelezaji wa mpango wa muda wa kati ambapo ujenzi wa (parallel/taxiway shoulders) utafanyika, ujenzi wa mahoteli, ujenzi wa maofisi ya kibiashara na ukamilishaji wa barabara za ndani. Awamu ya tatu ni utekelezaji wa mpango wa muda mrefu, awamu hii itahusu ujenzi wa barabara na madaraja kuzunguka mipaka ya nje ya kiwanja na ujenzi wa jengo la shughuli za usafiri wa anga, awamu hii itatekelezwa kupitia ushirikishwaji wa sekta binafsi.

Kuendelea kutenga maeneo ya uwekezaji kwa mfano Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetenga eneo la viwanda vikubwa huko Buhongwa viwanja 100, eneo

la Kabuhoro viwanda vidogo viwanja 20, mahoteli na burudani viwanja 8 huko Luchelele na viwanja vya makazi 700 huko Kiseke. Misungwi imetenga eneo la viwanda hekta 1,200 katika kijiji cha Nyang'homango.

Katika eneo la utalii , vivutio mbalimbali vimeainishwa kwa mfano Kisiwa cha Saanane kilichopo Jijini Mwanza, Kijereshi mbuga ya wanyama iliyopo wilayani Magu, Kituo cha zana na kumbukumbu za mila za wasukuma Bujora wilayani Magu, Kisiwa cha Rubondo chenye mbuga za wanyama wilayani Geita, Nyayo za Mwanamalundi Kwimba, jiwe linalocheza la Naburebeka wilayani Ukerewe, Jiwe la Bismark lililopo Jijini Mwanza. Pia, Mkoa unaendelea kutangaza vivutio hivyo kwa kushirikiana na Sekta binafsi mfano Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV).

Sekta ya Madini:

Wilaya ya Geita ni maarufu kwa uchimbaji wa dhahabu, uchimbaji huo unafanywa na Anglogold Ashanti inayomiliki Mgodi wa dhahabu Geita unaojulikana kama Geita Gold Mine (GGM) lakini bado yapo meneo mengine ya kuwekeza yenye madini kama Almasi huko Misungwi na Sengerema katika kijiji cha Lubaga na Satta ambako dhahabu pia inapatikana.

Sekta ya Uvuvi:

Eneo kubwa la Mkoa wa Mwanza ni maji ya Ziwa Victoria ambapo kuna maeneo mengi ya uwekezaji kama vile viwanda vya samaki. Mkoa unavyo viwanda 7 vya kuchakata samaki.

Sekta ya Nishati:

Mkoa hupata umeme wa gridi ya Taifa kupitia kituo kikuu cha umeme kilichopo Nyakato. Katika kuendeleza usambazaji wa Nishati ya umeme, kwa mwaka 2011 baadhi ya maeneo yatapata umeme kupitia mfuko wa changamoto za millenia (Millenium Challenge Cooperation). Baadhi ya maeneo yanayotegemea kupata

umeme ni Geita (Katoro, Nyang'hwale, Rwamugasa, Bukoli na Msalala), Misungwi (Nyamaiza na Seeke), Sengerema (Katungulu, Nyehunge na Nyamililo) na Ilemela jijini Mwanza.

**5.0 HITIMISHO:**

Ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake mkoa una dira, dhima na malengo. Aidha, dhana ya kupeleka madaraka kwa Umma (D by D) pamoja na dhana ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na uhuru kamili wa kujiamulia mambo yake siyo kigezo cha kutoa huduma mbovu kwa jamii ya watanzania. Mkoa unalo jukumu la kuhakikisha Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali Kuu inatekelezwa ipasavyo na Mamlaka za Serikali za Mtaa.

**TUMETHUBUTU, TUMEWEZA, TUNAZIDI KUSONGA MBELE**